

Rais Samia akamia kubana matumizi

- Ni kwenye bajeti ijayo ya Shilingi trilioni 62

Uk.
6&7



Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ili kuhakikisha rasilimali zilizopo zinatumika kwa ufanisi na kuzingatia vipaumbele vya taifa,”



Soma ndani

Serikali yafafanua malalamiko ya ‘Dudubaya’

Habari Uk. 17

Trump aingiwa mchecheto

RAIS wa Marekani, Donald Trump ameanza kupata mshawasha akihofia kuondolewa madarakani kabla hajamaliza muda wake wa miaka minne.

Hospitali ya Shifaa yaimarisha mapinduzi ya tiba Uk. 9

Profesa Mkumbo akemea mawaziri

WAZIRI wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo amewataka mawaziri na wakuu wa mikoa kuacha kujiona “mabosi wa kila mtu” wakiwamo wawekezaji pamoja na wafanyabiashara.

Uk.
15

Serikali yakwaa kisiki Ngorongoro

Uk.
12



■ Tahariri

Uokozi siyo ziada, ni wajibu wa serikali

HABARI ya kutokea kwa vifo sita vya wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma hakika imesikitisha Watanzania na wengine kujiuliza, hivi hakuna vifaa vya uokozi na wataalamu maneo yenye maji?

Gazeti la Pambazuko linahoji, iwe je watumishi hao sita wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma walifariki dunia kutokana na ajali ya boti, je, hakukuwa na uokozi wa wataalamu, hasa Jeshi la Zimamoto?

Inaelezwa kuwa ajali hiyo ilitokea baada ya boti yao kupinduka kufuatia upepo mkali walipokuwa wakielekea Kagunga kutoa huduma za afya, je, inawezekana je kwamba hawakupiga hata simu kupata msaada? Kwani upepo ulikuwa wa kimbunga?

Ajali hiyo hakika ni ukumbusho mchungu kwamba nchi yetu bado ina mapengo makubwa katika maandalizi, vifaa na wataalamu wa uokoaji.

Hapa ndipo sisi Pambazuko tunaposimama na kuitaka serikali kuongeza bajeti ya uokoaji na usimamizi wa majanga kwa kununua vifaa vya kisasa vya uokozi, na kuwekeza zaidi katika mafunzo ya wataalamu wa kukabiliana na dharura nchi nzima.

Hili siyo suala la hiari. Ni suala la kulin-da maisha, mali, rasilimali za umma na nguvu kazi ya taifa.

Ajali kama hizi zinapotokea, hasara yake haiishii kwenye machozi ya familia. Taifa hupoteza wataalamu waliofunzwa kwa gharama kubwa, huduma za umma huvurugika, na uchumi hubeba mzigo wa maafa ambayo mara nyingi yangepunguzwa kwa maandalizi bora ya kukabili majanga kila mahali.

Ni kweli Tanzania tayari ina mfumo wa kisheria na kimkakati. Mkakati wa Taifa

wa Usimamizi wa Maafa wa 2022–2027 unaeleza wazi kuwa nchi inaongozwa na Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022, pamoja na mpango wa maandalizi na mwitikio wa dharura unaolenga kujenga uwezo wa kuzuia, kujiandaa na kukabili majanga.

Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mratibu mkuu wa majanga.

Hata hivyo, sheria na mikakati pekee havitoshi kama havina meno ya bajeti, vifaa na watu wa kutosha wa kuvitekeleza kwa kasi na weledi.

Ndiyo maana bajeti lazima ionekane kwenye matokeo ya vitendo, boti salama za uokoaji katika maeneo ya maziwa na bahari, jaketi za kuokoa maisha, vifaa vya mawasiliano ya dharura, magari ya uokoaji, vifaa vya kutabiri na kufuatilia hali hatarishi, pamoja na vikosi vya wataalamu vilivyopo karibu na maeneo yenye hatari kubwa.

Inaonekana kwenye vitabu kwamba serikali tayari imetenga shilingi bilioni 18.013 kwa miradi ya maendeleo ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mwaka 2025/26, jambo linaloonyesha kuwa msingi upo; kinachohitajika sasa ni kuongeza kasi, kupanua wigo na kuhakikisha uwekezaji huo unaonekana mpaka ngazi za mikoa, wilaya na jamii zilizo pembezoni.

Somo la Kigoma linapaswa kuamsha dhamira mpya ya taifa, endapo kungekuwepo maandalizi bora zaidi, vifaa vya kutosha na wataalamu wengi wa uokozi, inawezekana baadhi ya vifo visingetokea. Serikali isi-subiri janga jingine ili ijifunze tena.

Pambazuko tunasisitiza kuwa suala la uokoaji wa kisasa, siyo gharama ya ziada; ni kinga dhidi ya hasara kubwa zaidi zinazoweza kuzuilika.

Lala Salama Ssebo... ■



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Paul Makonda akimfariji Cayden-William Busulwa, mtoto wa Mkurugenzi wa Uendeshaji na Biashara wa EFM na ETV, Denis Busulwa – almaarufu Ssebo katika ibada iliyofanyika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Martha, Mikocheni, Dar es Salaam. Ssebo alifariki dunia Machi 11, 2025 na mwili wake ulisafirishwa jana kwenda Uganda kwa ajili ya maziko. (Picha kwa hisani ya CMG).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Dunia: Hapa na pale

Uchumi duniani kudorora

VITA vya Marekani na Israel dhidi ya Iran, vi-naweka uchumi wa dunia kwenye hatari kubwa ya kuyumba kwa sababu vinatikisa moyo wa soko la nishati duniani.

Kufungwa kwa Mlango wa Hormuz, njia muhimu inayopitisha karibu sehemu kubwa ya mafuta na gesi ya kimiminika, tayari kumesa-babisha upungufu mkubwa wa usambazaji na kupandisha bei ya mafuta hadi zaidi ya dola 100 kwa pipa.

Bei hizo zikizidi kupaa, gharama za usafiri, uzalishaji wa viwandani, chakula na umeme zi-taongezeka kwa kasi katika nchi nyingi.

Hali hiyo inaweza kuchochea mfumuko wa bei, kupunguza biashara, kudhoofisha sarafu za nchi maskini na kuisukuma dunia kwenye mdororo wa uchumi, hasa ikiwa vita vitaende-lea na miundombinu zaidi ya mafuta itaharibi-wa.

Rais Museveni abanwa

WANA HARAKATI wa haki za binadamu nchini Uganda na nje ya nchi hiyo, wanaendelea kushinikiza Rais Yoweri Museveni kuhakikisha mwanasiasa wa upinzani, Kizza Besigye anaachiliwa huru.

Wanadai kuwa Besigye, ambaye amekuwa ru-mande tangu Novemba 2024, amekuwa kifungo-ni kwa kesi ya kubumba, hivyo aachiwe huru.

Mwito huo umeungwa mkono pia na baadhi ya taasisi za kimataifa, zikiwamo Jumuiya ya Madola na wabunge wa Ulaya, ambao wametaka aachiliwe mara moja.

Serikali ya Ugan-da imekuwa ikisisitiza kuwa mchakato wa she-ria unaendelea, lakini wanaharakati wanaamini shinikizo la kisiasa “kuto-ka juu” ndilo linalomwe-ka Besigye gerezani.



Bado shaka yazonga

BAADHI ya wananchi wa Venezuela wanautaza-ma utawala wa sasa kwa shaka baada ya kuondole-wa kwa Nicolas Maduro na vikosi vya Marekani Januari 2026.

Wengi bado wana hofu kuwa mfumo wa zama-ni wa ukandamizaji haujavunjwa kabisa kutokana na makamu wa zamani wa rais, Delcy Rodriguez, ndiye anayeshikilia uongozi wa mpito kwa mujibu wa katiba.



Serikali ya sasa imeahidi mageuzi ya kisiasa, msama-ha kwa baadhi ya wafung-wa na kufungua uchumi kwa wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, ujumbe wa Umoja wa Mataifa umese-ma taasisi zilizotuhumiwa kwa ukiukwaji wa haki za binadamu bado zinaende-lea kuzongwa.

Malaysia yapaa zaidi

UCHUMI wa Malaysia unaendelea kuwa mfa-no wa kuigwa baada ya kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2025, ukichochea na kubana ma-tumizi, utalii, huduma na viwanda.

Serikali ya nchi hiyo imeendelea kulisitiza nidhamu ya matumizi ya umma, uwazi wa ut-awala na usimamizi bora wa rasilimali kupitia Mpango wa 13 wa Malaysia na sheria ya uwaji-bikaji wa fedha za umma.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) limese-ma nakisi ya bajeti ilishuka kutoka asilimia 4.1 ya pato la taifa mwaka 2024 hadi asilimia 3.8 mwaka 2025, jambo linaloonyesha uimara wa sera zake za kifedha.

Mwelekeo huo unaifanya Malaysia kutajwa kuwa nchi ambayo ukuaji wake unajengwa juu ya uongozi wenye nidhamu, uzalishaji na mi-pango ya muda mrefu

Na Mzee TAI



Jicho la Tai

Kamari kisima cha kumeza fedha

LEO mzee wenu nimeamka na maumivu ya mgongo na kijihoma, ingawa nasikia kichwa nacho kinagonga. Najua ni uzee, maana viungo – katika umri mkubwa kama wangu, huanza kukataa kutiili amri ya akili.

Pamoja na changamoto hiyo ya afya, nimeamua kuita vijana wa mtaani na kuwapa somo la maisha; kubwa ikiwa ni kuwahimiza kuacha michezo ya kamari, maana naona na nimeambiwa wengi wameingia kucheza madubwi.

Katika kikao chetu, nimeamua kubeba filimbi mkononi, siyo kwa ajili ya kuanza mechi, bali kusimamisha huu mchezo wa kuteketeza hela uitwao kamari.

Maana yake nini? Kijana anaamka asubuhi hana sabuni, lakini ana bando la kutosha kubeti mechi za Honduras, Croatia na ligi ya watu wanaocheza mpira na theluji. Hapo kweli tunajenga taifa au tunafungua tawi jipya la majonzi?

Kamari imewageuza baadhi ya vijana kuwa wataalamu wa “karibu nitoboe.” Kila siku ni maneno yaleyale, “mzee leo nimeiona kabisa!” Ukiuliza ameona nini, utagundua ameona giza tu. Hela ya vocha inaingia kwenye mkeka. Nauli ya kwenda kazini inaingia kwenye ‘odds. Fedha ya kula mchana inawekwa kwenye “both teams to score.”

Mwisho wa siku tumbo linapiga yowe, mfuiko unalia, halafu kijana anasema bahati haikuwa yake. Bahati gani, wakati hata kuku wa jirani ana maisha ya uhakika kuliko wewe?

Tatizo kubwa zaidi ni kwamba kamari iki-shika shingo, kijana anaanza kubadilika tabia. Akikosa hela ya kubeti, anaiba kijiko nyumbani, kesho pasi ya umeme, keshokutwa sufuria. Vikiisha, macho yanaanza kutazama mali za jirani kwa upendo wa ajabu.

Hapo ndipo mchezo wa mkeka unavyozaa mchezo wa mahabusu. Kijana kutoka “banker” anaishia kuwa “burglar.” Hiyo siyo akili, ni tiketi ya bure kwenda kuharibu maisha.

Mimi sisemi vijana wakae tu kama sanamu wakisubiri miujiza ishuke kutoka mawinguni. Hapana. Fursa zipo, ingawa haziji kwa ngoma.

Mnaweza kuwa watengeneza maudhui, wapi-ga picha, waandishi wa mtandaoni, mafundi simu, wauza juisi, wachomaji mihogo, wao-sha magari, hata wauza mitumba kwa akili na nidhamu.

Serikali nayo inapotoa mikopo au mitaji kwa vijana, vikundi na wanawake, hizo ni nafasi za kushikwa kwa mikono miwili, siyo za kugeuzwa fedha za kubeti mechi za England.

Kijana mwenye akili anatengeneza chanzo cha kipato; hajengi taifa la kukariri takwimu za wapiga kona. Nchi haiendelei kwa odds, in-aendelea kwa kazi.

Hatuwezi kuwa taifa la vijana wanaojua zaidi orodha ya wafungaji kuliko orodha ya fursa za kujiajiri. Tujenge taifa la wabunifu, siyo la wabashiri wa mipira ya Ulaya, Hispania, Uholanzi na hata Israel.

Kwa hiyo, vijana wangu, achaneni na kamari kabla kamari haijawamaliza. Mkeka haujawahi kujenga nyumba, lakini umebomoa nyingi.

Mara nyingi ninasema; tafuteni kazi, jenge-ni vipaji, shikeni fursa, acheni kujenga taifa la wacheza kamari kana kwamba ubashiri ni ajira rasmi.

Huko mbele kuna maisha mazuri, lakini ha-yapatikani kwa kubeti, yanapatikana kwa jasho.



■ Habari Kuu

Rais Samia akamia kubana matumizi



Rais Samia Suluhu Hassan

Na Mwandishi WETU

SERIKALI inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inapanga kukusanya na kutumia shilingi trilioni 62.33 katika mwaka ujao wa fedha, likiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 kulinganisha na bajeti ya sasa ya shilingi trilioni 56.49.

Ili kuzipata fedha hizo na kuhakikisha zinatumika ipasavyo, serikali imeainisha mipango kadhaa iliyowekwa wazi jijini Dodoma wiki iliyopita na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Musa Omar, kupitia mpango wa ukomo wa bajeti aliuwasilisha kwa wabunge.

Katika mipango ya bajeti hiyo ambayo ni ya kwanza katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, serikali imesema kuwa itaweka mkazo katika nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, kuongeza mapato ya ndani, kuimarisha sekta binafsi na kuendeleza miradi ya maendeleo.

Mipango hiyo imewafurahisha baadhi ya wachambuzi wa uchumi wanaosema kuwa inaonyesha mwelekeo wa serikali ni kulinda uthabiti wa uchumi ambao umeanza kuimarika.

Aidha, wanasema iwapo zitatekelezwa kikaamilifu hatua hizo zitachochea ukuaji wa uchumi wa muda wa kati na mrefu.

Lakini, wameonya kuwa ili hayo yatokee, ni vyema serikali ikawa na nidhamu ya kutekeleza inachoahidi na pia kuhakikisha inaendana na mabadiliko ya Uchumi wa Afrika na dunia kwa ujumla.

Akiwasilisha hotuba ya makadirio na ukomo wa bajeti ijayo, Waziri wa Fedha, Balozi Omar, amesema serikali itaendelea kuhakikisha matumizi ya fedha za umma yanazingatia vipaumbele vya maendeleo na nidhamu ya kifedha.

“Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ili kuhakikisha rasilimali zilizopo zinatumika kwa ufanisi na kuzingatia vipaumbele vya taifa,” alisema.

Hata hivyo, wachambuzi wa uchumi wanasema hatua hiyo ni muhimu lakini inahitaji ufuatiliaji makini ili kuhakikisha taasisi za umma zinazingatia mipaka ya matumizi.

Wachambuzi wanabainisha kuwa changamoto kubwa katika bajeti nyingi za serikali imekuwa siyo sera bali utekelezaji wake.

“Serikali imekuwa ikiweka msisitizo wa nidhamu ya matumizi kila mwaka, lakini changamoto imekuwa katika kuhakikisha taasisi za umma zinazingatia kikamilifu mipaka ya bajeti. Bila usimamizi madhubuti, nakisi ya bajeti inaweza kuendelea kuongezeka,” alisema mmoja wa wachambuzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye hakupenda jina lake litajwe.

Maeneo ya kipaumbele

Moja ya maeneo makubwa yanayopewa kipaumbele katika bajeti ya 2026/27 kwa mujibu wa Waziri Omar ni uwekezaji katika miradi ya maendeleo, hasa katika sekta za miundombinu, nishati, maji, afya na elimu.

Inaendelea Uk.7

Habari Kuu ■

Samia akamia...

Inatoka Uk. 6

Waziri huyo wa fedha alisema uwekezaji huo ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma kwa wananchi na pia kuendelea miradi ambayo tayari ilishaanzishwa.

“Serikali itaendelea kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya maendeleo ambayo inalennga kuimarisha miundombinu, kuongeza tija ya uzalishaji na kuchochea ukuaji wa uchumi,” alisema.

Hadi hivi sasa uwekezaji katika miundombinu umechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi katika miaka ya hivi karibuni, ingawa baadhi ya miradi bado haijakamilika.

Lakini wachambuzi wanaonya kuwa ufanisi wa miradi hiyo unapaswa kupimwa kwa matokeo yake katika uchumi halisi na si maneno ya kisiasa pekee kama “tuliahidi, tumetekeleza.”

Mtaalamu wa uchumi kutoka taasisi ya Policy Forum, anasema uwekezaji katika miundombinu ni muhimu lakini lazima uendane na tija ya kiuchumi.

“Miradi mikubwa ya miundombinu inaweza kuchochea uchumi ikiwa itaongeza tija katika sekta nyingine kama viwanda, biashara na kilimo. Lakini kama haitazalisha shughuli za kiuchumi, inaweza kuongeza mzigo wa deni,” alisema mtaalamu huyo.

Kupunguza utegemezi

Jambo jingine lililojitokeza katika bajeti hiyo ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza Julai Mosi mwaka huu ni mkazo mkubwa ulioyekwa katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa lengo la kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo kutoka nje.

Hilo lilitarajiwa na watu wengi hasa baada ya misaada kutoka nje kuanza kupungua kutokana na kashfa ya vurugu za kisiasa zilizoandamana na uchaguzi mkuu uliopita, ambazo zimeharibu taswira ya nchi nje.

Ili kulifanikisha hilo, Waziri wa Fedha anasema serikali itajikita katika kupanua wigo wa walipa kodi na kuimarisha mifumo ya uku-



Waziri wa
Fedha, Balozi
Khamis Mussa
Omar

sanyaji mapato kwa kutumia teknolojia za kidigitali ili kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa wingi.

“Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa walipa kodi, kuimarisha usimamizi wa kodi na kutumia mifumo ya kisasa ya kidigitali,” alisema.

Kwa mujibu wa wataalamu wa uchumi, kuongeza mapato ya ndani ni hatua muhimu katika kujenga uchumi unaojitegemea, lakini wanaonya kuwa hatua hiyo lazima izingatie uwezo wa sekta binafsi.

Hata hivyo, wachambuzi wanaishauri serikali kuwa inapaswa kuwa makini katika mipango ya kuongeza wigo wa kodi kwani kuna hatari ya kuwaingiza watu ambao hawana uwezo mkubwa wa kulipa kodi.

Matokeo yake, wanasema Tanzania inaweza kuwa na idadi kubwa ya walipa kodi lakini makusanyo yakawa madogo.

Sekta isiyo rasmi

Aidha, mipango hiyo inahatarisha ustawi wa sekta isiyo rasmi ambayo kwa kiasi kikubwa hivi sasa haijaingizwa kwenye wigo wa ulipaji kodi.

Inaendelea Uk.8

■ Habari Kuu

Samia akamia...

Inatoka Uk. 7

Harakati za kuingiza sekta hiyo katika wigo wa kodi unaweza kuleta madhara kwani kwa kiasi kikubwa sekta isiyo rasmi inaundwa na watu ambao hawana uhakika wa kipato.

“Kupanua wigo wa walipa kodi ni muhimu, lakini serikali lazima ihakikishe kuwa hatua hizo haziongezi mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ambao tayari wanakabiliwa na changamoto za gharama za uzalishaji,” alisema mmoja wa wachambuzi hao.

Katika hotuba yake, Waziri Omar anabainisha kuwa serikali inalenga kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kukuza sekta binafsi kama injini ya ukuaji wa uchumi.

Waziri wa Fedha anasema serikali itaendelea kuboresha sera na miundombinu ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

“Sekta binafsi inaendelea kuwa mshirika muhimu wa serikali katika kukuza uchumi, hivyo serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ili kuvutia mitaji na teknolojia,” anasema.

Utambuzi wa sekta binafsi kama moja ya makundi ya kuwezesha ukuaji wa uchumi

umetambuliwa pia katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Hata hivyo, ili serikali ifanikishe hili inahitaji kutatua changamoto zinazohusiana na urasimu na gharama za kufanya biashara, mambo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wafanyabiashara kutoka sekta binafsi kwa muda mrefu.

Wachambuzi wanasema mazingira ya uwekezaji yataboreka zaidi ikiwa serikali itapunguza urasimu katika utoaji wa vibali na huduma kwa wawekezaji.

Wachambuzi wanabainisha kuwa wawekezaji wanahitaji mazingira yenye uhakika wa sera, urahisi wa kufanya biashara na mifumo ya haraka ya maamuzi.

Kilimo, uzalishaji, viwanda

Aidha, bajeti ya 2026/27 inaendelea kuisisitiza maendeleo ya sekta za uzalishaji kama kilimo, viwanda, madini na utalii, ambazo zinakonekana kuwa nguzo muhimu za uchumi wa Tanzania.

Serikali inaamini kuwa kuimarisha sekta hizo kutasaidia kuongeza ajira, kuongeza uzalishaji na kukuza mauzo ya nje.

Waziri wa Fedha alisema serikali itaendelea kuwekeza katika sekta hizo ili kuongeza thamani ya bidhaa za ndani na kukuza ushindani wa Tanzania katika masoko ya kimataifa.

“Lengo letu ni kuimarisha sekta za uzalishaji ili ziweze kuongeza thamani ya bidhaa za ndani, kukuza ajira na kuongeza mapato ya taifa,” alisema.

Hata hivyo, serikali imeshauriwa kuboresha mazingira ya uzalishaji, hususan katika upatikanaji wa nishati, mitaji na teknolojia, ili kukuza uzalishaji hasa kutoka sekta binafsi.

Kwa ujumla, wachambuzi wanasema mfu-mo na ukomo wa bajeti ya 2026/27 unaonyesha juhudi za serikali kuimarisha uthabiti wa uchumi huku ikichochea ukuaji wa muda mrefu.

Hata hivyo, wanasema mafanikio yake yatategemea zaidi utekelezaji wa sera hizo na uwezo wa taasisi za serikali kusimamia rasili-mali za umma kwa ufanisi.



Shifaa yaimarisha mapinduzi ya tiba

Na Mwandishi WETU

HIVI karibuni idadi ya Watanzania wenye changamoto ya afya wanaosafiri kwenda ughaibuni kwa matibabu, huenda ikapungua sana kutokana na kuwepo kwa huduma za kisasa na vifaa tiba vya kisasa.

Moja ya hospitali inayoelezwa kuchangia kupungua kwa wagonjwa kwenda nje kusaka tiba ni uwepo wa Hospitali ya Shifaa ya jijini Dar es Salaam ambayo imeendelea kudhihirisha mabadiliko makubwa katika sekta ya afya nchini baada ya juzi kuzindua kitengo kipya cha tiba, ushauri na mafunzo kuhusu magonjwa ya mfumo wa upumuaji.

Uzinduzi wa kitengo hicho unaonekana kuwa sehemu ya mageuzi yanayokwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wanapata matibabu yenye ubora wa hali ya juu kwa gharama nafuu ndani ya nchi, badala ya kulazimika kusafiri nje kutafuta huduma hizo.

Kwa takribani miaka miwili tangu hospitali hiyo ianze kutoa huduma, Shifaa imejijengea sifa kuwa moja ya vituo vya tiba inayowekeza zaidi katika vifaa tiba vya kisasa, wataalamu wabobezi pamoja na wasaidizi wa afya wenye ujuzi unaoendana na mahitaji ya sasa ya tiba.

Kitengo hicho kipya kinatarajiwa kusaidia kwa kiasi kikubwa uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya mfumo wa upumuaji ambayo yamekuwa yakisumbua watu wengi, wakiwamo watoto, wazee na wagonjwa wenye changamoto za muda mrefu za kiafya.

Mbali na tiba, kitengo hicho kitatoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo yanayolenga kuongeza uelewa wa jamii pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya.

Hatua hiyo pia inatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya Watanzania wanaosafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya magonjwa yanayohitaji utaalamu na teknolojia ya hali ya juu.

Hili lina maana kubwa siyo tu kwa ustawi wa



wagonjwa na familia zao, bali pia kwa uchumi wa taifa kupitia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Shifaa, Bashir Haroon, aliishukuru serikali kwa ushirikiano wake na utayari wa kusaidia mambo mbalimbali yanayohitajika kuimarisha sekta ya afya kupitia hospitali binafsi.

Bashir alisema mazingira mazuri ya ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi ni muhimu katika kuharakisha upatikanaji wa huduma bora, kuongeza uwekezaji wa vifaa na utaalamu, na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha tiba ya kisasa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kupitia hatua hiyo, Shifaa inaendelea kuwa ishara ya matumaini mapya katika huduma za afya nchini.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

Kwenye amani kuna utulivu, kinyume chake siyo lazima



NIMESIKIA serikali ikisisitiza kuwa Tanzania sasa ni tulivu na kila kitu kiko sawa. Tamko hili tamu sana, lakini kuna haya, yatusaidie kuto-fautisha utulivu na amani.

Sijamsikia kiongozi yeyote wa juu wa serikalini akiongelea utekaji, utesaji, na mauaji. Hata kwa kuigiza, atokee kiongozi alaani vitendo hivi.

Nimesikia baadhi ya viongozi wakiongea kwa mafumbo kama ninavyoongea mimi kwamba “lile lililotokea nchini kwetu Oktoba 29...” Wanasita hata kulitamka ni jambo gani. Litamkwe ili taifa lipone.

Kuna mivutano mingi kati ya taasisi kadhaa na serikali. Mivutano hiyo haijengi. Chanzo twaweza kukijua, lakini matokeo yake hatuyajui. Tulidhani Wakatoliki “vijora” ni wa kike, kumbe na wanaume vijora wapo?! Kwaresima ifute vijora wote.

Kwa kuwa hakuna anayeongelea utekaji na kutueleza waliotekwa wako wapi, basi angalau fanyeni haya ili tujue kuna amani na siyo utulivu tu.

Kwanza, acheni watu watekwe lakini wawe

huru kusema kuwa wametekwa. Watekaji wawe na haki ya kuteka; na watekwaji na jamaa zao wawe huru kupiga kelele.

Pili, watu wafichwe vituo vya polisi vilivyo rasmi na visivyo rasmi bila taarifa, lakini ndugu zao wawe huru kupiga kelele kuwa ndugu zao wamefichwa.

Tatu, watu wabambikiwe kesi, lakini wao na ndugu zao wawe huru kusema wanavyobambikiwa kesi.

Nne, viongozi wawaudhi wananchi na wananchi wawe huru kununa.

Tano, watu waambiwe kwamba kabla hawa-jaongea na vyombo vya habari wapite serikalini kupatiwa cha kusema, vinginevyo watakutana na Ithibati (siyo hisabati).

Sita, watu wawapigie ‘makofi’ viongozi, lakini wawe huru kusema kuwa wameagizwa washangilie na kupiga makofi.

Saba, wananchi wawe huru kusema hapakuwa na uchaguzi, lakini nchi haiwezi kukaa bila rais kwa hiyo aliyekuwepo anaendelea.

Nane, wananchi wawe huru kusema uchaguzi ulikuwepo, lakini ukavurugwa na kuvuruga matokeo yanayohojiwa. Nchi haiwezi kukaa bila rais. Ndiyo maana yanatafutwa maridhiano kujua kama uchaguzi ulikuwepo au haukuwepo ili tujue tunatokaje.

Tisa, wananchi wawe huru kusema kuwa bunduki inaleta utulivu, lakini uhuru unaleta amani. Ndani ya amani kuna utulivu, lakini si kila utulivu una amani.

Kumi, serikali yetu iige hekima ya Kijaluo kwamba, mengine yote tunayo hapa nchini ila kinachokosekana ni uhuru. Kwamba serikali isiporejesha uhuru, na yenyewe haitakuwa huru. Badala ya kupigiwa makofi, itapigwa makofi.

Mjaluo amehesabu na kugundua kuwa vidhibiti uhuru vimezidi kuwa vingi. Sasa hata wenye magari ya mikopo na ya kuazima yenye namba “A,” mwisho wake ni Kisarawe, Mkuran-ga, Mlandizi na Bagamoyo. Serikali itawalipia mikopo yao lakini magari yabaki nje ya jiji!

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Iko wapi roho ya harakati za wanawake?

MACHI 8 ni maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka. Siku hii imetokana na mapambano ya haki za mwanamke.

Wanawake walitambua kuwa haki haiombwi, bali hutafutwa pale inapokuwa imepokonywa.

Wanawake walianza kupambana hadi kufikia utambuzi wa haki zao kuwa haki za binadamu.

Pamoja na utambuzi huo, bado kumekuwa na sababu ya wanawake kuwa na maadhimisho ambayo yanawapa fursa kutambua vikwazo walivyoruka kwa mafanikio na vikwazo ambavyo bado virefu.

Ni siku ya kushangilia huku wakiweka mikakati ya kuendeleza heshima ya kila mtu. Maadhimisho haya siyo ya baadhi ya wanawake, ni kwa wanawake wote, ili kuwavuta pamoja kupambania haki.

Maadhimisho ya mwaka huu yaliadhimishwa wiki iliyopita sehemu mbalimbali duniani na hata hapa nchini.

Nilivyokuwa nafuatilia namna yalivyoadhimishwa hapa nchini, nilipata maswali kadhaa moja ikiwa ni je bado tunaishi katika roho ile ile ya harakati za wanawake zenye lengo la kuwaleta wanawake pamoja bila kujali tofauti zao?

Je, ile roho ya kuwa mlinzi wa dada yako ipo bado au kila mtu ajijue mwenyewe?

Swali hili limejitokeza baada ya kuona jinsi wanawake wa Chadema, walivyozuiwa kufanya maadhimisho. Ilifika mahali wengine waliweka rumande na wengine kupigwa mabomu ya machozi walipokuwa wakijiandaa kufanya maadhimisho hayo.

Kwa tafakari yangu, niliona kilichofanywa na Jeshi la Polisi siyo sahihi.

Nilimsikia askofu wa huko Musoma akikemea tukio lile la mabomu kurushwa katika eneo la kanisa ambapo liliathiri hata watoto na wazee.

Nilisikia ufafanuzi wa kisheria uliotolewa na Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), akisema hapakuwa na sababu yoyote ya kisheria kuwazuia wanawake wale kuadhimisha siku yao.

Nilitamani sana kuona na kusikia sauti pana zaidi ya wanawake wote kukemea jambo hilo na



Rais wa TLS,
Boniface
Mwabukusi

kusimama na hawa wanawake waliopata adha wakati wakijaribu kuadhimisha siku hii.

Bahati mbaya sikuisikia sauti ya pamoja nikazidi kutafakari na kuona huenda sauti hiyo haikuwepo kwa vile walioathirika ni wa chama cha siasa pamoja na kuwa ni wanawake.

Jambo tunalotakiwa kulijua ni kuwa iwapo mwanamke mmoja atavunjiwa haki na wanawake wengine tukawa kimya, maana yake ni kuwa tunaalika uvunjifu wa haki kwa mwanamke mwingine.

Katika maadhimisho haya niliwasikia wanawake wakizungumzia kwa maumivu jinsi ukatili wa kijinsia unavyoendelea nchini.

Walitazama masuala ya ubakaji, ulawiti na vipigo. Ni kweli haya ni mambo mabaya ya kukemewa kabisa na tukiwa katika kukemea hayo tutambue kuzuiwa kuadhimisha siku ya wanawake nao ni ukatili kwa wanawake.

Polisi wamewakosea wanawake siku hii ni tendo tunalolilaani. Wanawake tusikubali kugawanywa kwa sababu yoyote. Macho yawe katika haki za wanawake wote popote.

Tukikaa kimya, kwa hakika tunaiua roho ya harakati za mwanamke. Maadhimisho haya yatakosa maana yasipotusukuma kusema ukweli tukiwa pamoja.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

■ Habari

Serikali yakwaa kisiki Ngorongoro



Na Mwandishi WETU

SERIKALI, imekwaa kisiki katika zoezi la kuwahamisha kwa hiari wafugaji wenye asili ya kimasai, wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro wanaoishi katika Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), mkoani Arusha.

Hali hiyo imejidhihirisha wiki iliyopita, wakati Mwenyekiti wa Tume ya Kutathmini Uhamaji wa Hiari Ngorongoro, Mussa Iyombe, alipokuwa akiwasilisha ripoti ya tume hiyo, mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Desemba 23, mwaka 2024, Rais Samia aliunda tume mbili ikiwamo iliyoongozwa na Iyombe na nyingine iliongozwa na Jaji Mstaafu, Gerad Ndika, kwa ajili ya kutathmini matumizi ya ardhi Ngorongoro.

Tume hizo ziliundwa baada ya uwepo wa malalamiko ya muda mrefu juu ya matumizi ya ardhi kwa wakazi wa Ngorongoro ambayo yalisababisha serikali ianzishe zoezi la kuwahamisha kwa hiari wakazi wa eneo hilo mwaka 2022, kwenda katika maeneo ya Msomera, Handeni, Tanga, Sauni, Wilaya ya Kilindi, Tanga na Kit-

wai B, iliyoko Simanjiro, Manyara.

Katika taarifa yake mwishoni mwa wiki kwa niaba ya wajumbe wanane wa tume hiyo, Iyombe alisema licha ya serikali kuwa na nia njema ya zoezi hilo, uhamaji huo haukufanikiwa kama ilivyotarajiwa kwa kuwa idadi kubwa ya kaya na mifugo zilizotakiwa kuhama, hazikuhami.

Alisema kwamba, hadi sasa nyumba 1,559 zilizojengwa na serikali katika Kijiji cha Msomera kwa ajili ya wananchi waliotarajiwa kuhama kwa hiari kutoka Ngorongoro, ziko tupu kwa kuwa wananchi wamegoma kuhamia huko.

Wakati wa zoezi hilo ambalo serikali ilitumia gharama kubwa, Iyombe alisema zilihama kaya 1,678, sawa na asilimia 5.7, kati ya kaya 23,000 zinazoishi katika eneo la Ngorongoro.

Kwa mujibu wa Iyombe, licha ya serikali kutenga shilingi bilioni 212.35 kwa ajili ya uhamaji wa hiari, imeshatumia shilingi bilioni 18.59 kujenga nyumba na miundombinu Kitwai B, shilingi bilioni 15.89 kujenga nyumba na miundombinu Sauni na ilitumia shilingi bilioni 114.36 kujenga nyumba na miundombinu katika Kijiji cha Msomera.

Kuhusu mifugo iliyohamishwa, alisema ilitumia mifugo 40,593, sawa na asilimia 5.7 ya mifugo 715,466, iliyokuwa ikifugwa katika eneo hilo wakati zoezi la uhamaji lilipoanza.

Kwa kifupi, zoezi la uhamaji wa hiari limekwama ndiyo maana serikali inajipanga upya ili ione ni kwa jinsi gani itafikia malengo yake ya kuwahamisha wafugaji hao.

Kutokana msimamo huo wa wamasai, maswali ya kujiuliza yamekuwa mengi kuliko majibu yanayopatikana baada ya zoezi hilo kukwama.

Maswali ni mengi kwa sababu wakati zoezi hilo linaanza, serikali iliamini ingefanikiwa, lakini, imejikuta ikigonga mwamba licha ya kutumia ushawishi na mabilioni ya fedha za walipa kodi.

Inaendelea Uk. 13

Serikali yakwaa...

Inatoka Uk. 12

Kila kundi la wafugaji hao lilipokuwa likiha-ma Ngorongoro, serikali ilikuwa ikitumia vyombo vya habari kuhakikisha tukio hilo linatangazwa vilivyo ili kuona ni kwa jinsi gani wafugaji hao walivyotii ushauri wa serikali.

Watu maarufu, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini na viongozi wa serikali, walikuwa wakishiriki kwa njia tofauti, kuhamasisha uhamaji huo wa hiari ambao sasa tunaeleza haukufanikiwa.

Katika maeneo waliyokuwa wakihamia wafugaji hao, serikali iliweka huduma zote muhimu kama maji, barabara zinazopitika, zahanati, shule za msingi na sekondari, umeme, masoko, viwanja vya michezo na majosho ya kuoshea mifugo.

Wahamaji walikuwa wakipewa nyumba bora za kisasa, walikuwa wakipewa motisha ya shilingi milioni 10, ekari tano za kilimo na ekari tatu za makazi.

Hata hivyo, pamoja na serikali kufanya yote hayo na mengineyo kwa nia njema, bado haikuweza kuwashawishi wamasai wahame Ngorongoro na kwenda katika maeneo waliyotengewa.

Wamasai wamegoma kuhama, wamekubali kuendelea kuishi Ngorongoro ambako mara kadhaa wanaumizwa, wanajeruhiwa na wengine wanauawa na wanyama wakali.

Baada ya kuona kasi ya uhamaji ni ndogo, serikali ililazimika kubadili gia kwa kuwawekea vikwazo wakazi wa Ngorongoro, waliokuwa wakisita kuhama makazi yao.

Taarifa zilizolifikia Pambazuko mwaka juzi, zilionyesha huduma za maji zilianza kudorora ikiwamo katika Shule ya Sekondari Laitole ambako chanzo chake cha maji kilitelekezwa na kusababisha wanafunzi wa shule hiyo, waanze kufuata maji katika Shule ya Sekondari ya Wasi-chana Ngorongoro iliyoko umbali wa kilomita moja.

Taarifa hizo zilisema serikali iligoma pia kukarabati majengo mawili ya nyumba za walimu katika Shule ya Msingi Esele yaliyokuwa yamee-

Watu maarufu, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini na viongozi wa serikali, walikuwa wakishiriki kwa njia tofauti, kuhamasisha uhamaji huo wa hiari...

zuliwa na upepo mwaka 2023. Pia serikali ilisita kukarabati jengo la Zahanati ya Esele ambalo lilikuwa linavuja kila mvua ilipokuwa ikinyesha.

Hata choo cha wanafunzi katika Shule ya Msingi Oldoinyo kilichokuwa na hali mbaya, hakikujengwa upya na jengo la darasa moja lililokuwa limejengwa kwa nguvu za wananchi katika Shule ya Msingi Oldoinyo, halikukamilishwa. Shule ya Msingi Enduleni iliyokuwa na uhaba wa vyoo, haikusaidiwa kutatua tatizo hilo, badala yake, wanafunzi 1,876 wa shule hiyo, walikuwa wakitumia matundu manane ya vyoo.

Katika shule hiyo iliyokuwa na mabweni mawili ya wanafunzi wa kike na wa kiume, zilikuwa zimetumika shilingi milioni 800 kukarabati mabweni hayo mwaka 2021 na kiasi kingine cha fedha kilichobaki, inasemekana hakikupelekwa tena.

Shule shikizi iliyokuwa imejengwa katika Kitongoji cha Kayapsi, ililazimika kusimama kwa miaka mitatu ingawa ujenzi wa jengo ulikuwa umekamilika, wakati Shule ya Msingi Oloilobi na Mokilali, vyoo vilikuwa vimejaa na havikujengwa vipya.

Pamoja na madhira hayo katika sekta ya elimu, miradi mingine ya maendeleo iliyokuwa imepangwa na iliyokuwa ikitekelezwa katika Tarafa ya Ngorongoro, ilisimama kwa miaka kadhaa kama sehemu ya shinikizo la wafugaji hao kuhamia Msomera, Kitwai B na Saunyi.

Katika sekta ya maji, wananchi walianza kukosa maji ya uhakika kwa kuwa pampu za kusukuma maji zilipokuwa zikiharibika, zilikuwa hazitengenezwi.

Kwenye sekta ya afya, huduma za afya zilianza kusuasua katika zahanati na vituo vya afya kikiwamo Kituo cha Afya Osiloni ambacho fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili yake mwaka 2022, hazikupelekwa tena.

Inaendelea Uk. 14

■ Habari

Serikali yakwaa...

Inatoka Uk. 13

Aidha, wananchi waliwekewa zuio la kupita katika eneo la NCAA baada ya saa 12 jioni na pia magari ya kampuni zilizokuwa zikitaka kutekeleza miradi ya maendeleo, ilinyimwa vibali vya kuingia NCAA.

Mwaka 2024, miezi michache kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofayika mwishoni mwa mwaka huo, majina ya wakazi wa Ngorongoro yalihamishiwa Msomera ili wakapigie kura huko ingawa wao walikuwa wakiishi Ngorongoro.

Uamuzi huo uliibua hasira za wafugaji hao ambapo Agosti, mwaka 2024, mamia ya wafugaji hao, walikusanyika katika Kijiji cha Kayoposi, Barabara ya Serengeti, wakipinga kuhamishwa na kutakiwa wakapigie kura Msomera.

Baada ya siku nne za wananchi hao kukusanyika, serikali iliwatuma viongozi waandamizi wakiongozwa na kada wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Abdallah Bulembo, kwenda Ngorongoro kukutana na wananchi hao.

Katika majadiliano yao, Bulembo na timu yake waliwahakikishia wananchi hao, kwamba Rais Samia anawathamini watanzania wote na kwamba zoezi la kuwahamisha kwa hiari katika makazi yao, linafanyika kwa nia njema na siyo kuwaumiza wananchi.

Wengine waliokwenda Ngorongoro ni aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Paramagamba Kabudi, aliyeongozana na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, William Lukuvi.

Hata hivyo, vikwazo hivyo havikuwayumbisha na wala havikuwakatisha tamaa wafugaji hao, badala yake waliendelea na msimamo wao wa kutohama makazi yao na kuifanya serikali ilegeze kamba kwa kurejesha huduma zote zilizokuwa zimesimamishwa.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Maendeleo Ngorongoro, Murtallah Mbillu, aliiambia Pambazuko, Agosti 30, mwaka 2024, kwamba serikali ilikuwa ikiyafanyia kazi malalamiko ya wa-

nanchi.

Katika maelezo yake wiki iliyopita, Iyombe alizitaja sababu mbalimbali zilizochangia wakazi wa Ngorongoro kutohama kwa hiari, kuwa ni zoezi kutowashirikisha wananchi ipasavyo.

Alisema kwamba, badala ya serikali kuwashirikisha wakazi hao, yenyewe ilikuwa ikiwashawishi wahame.

Licha ya kusema uhamaji wa wakazi hao ni muhimu na hautakiwi kusitishwa, elimu itolewe kwa wananchi, viongozi wa dini, viongozi wa serikali na kwa viongozi wa kisiasa.

“Utafiti wetu unaonyesha kwamba, wengine ambao ni muhimu katika kupewa elimu ni viongozi wa kimila maarufu kama maraigwanani. Hawa maraigwanani wanasikilizwa sana na wananchi na wasipopewa elimu na kuielewa sawasawa, jamii nzima haitaelewa pia,” alisisitiza Iyombe.

Hata hivyo, kauli hiyo inapingana na kauli iliyotolewa mwaka 2023 na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana, aliyesema kwamba, zoezi la uhamaji wa hiari Ngorongoro lilikuwa shirikishi kwa kuwa wananchi wote wa eneo hilo, walishirikishwa ipasavyo.

Rais Samia alipokuwa akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, aliahidi kuyafanyia kazi mapendekezo ya tume hiyo ili zoezi hilo lifanikiwe zaidi kwa kuwa ni endelevu.

Alimwagiza Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba na ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi, kuyafanyia kazi mapendekezo yote yalitotolewa na tume hiyo.

Wakati huo huo, mmoja wa viongozi wa kimila waishio Ngorongoro, aliiambia Pambazuko kwa sharti la kutotajwa jina lake jana, kwamba wakazi wa Ngorongoro wamefurahia uamuzi wa serikali wa kukubali kuwashirikisha wananchi kabla ya kuwahamisha.

Aidha, alitaka wanaume waliohamia Msomera na kupewa nyumba moja wakati wana wanawake zaidi ya mmoja, waongezewe nyumba kulingana na ukubwa wa familia zao.

Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche, aliiambia Pambazuko jana kwamba, watazungumzia ripoti ya tume hiyo wakati wowote baada ya kufanya utafiti wa kina.

Profesa Mkumbo akemea mawaziri

Na Mwandishi WETU

WAZIRI wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo amewataka mawaziri na wakuu wa mikoa kuacha kujiona “mabosi wa kila mtu” wakiwamo wawekezaji pamoja na wafanya-biashara.

Amesema mpango wa maendeleo wa miaka mitano unawataka viongozi hao kuweka mazingira ya biashara kwa kujipunguzia mamlaka ya udhibiti na kuruhusu miradi mbalimbali kufanywa na serikali za mitaa.

Mbali na hilo, Profesa Kitila (pichani) amesema hatarajii kusikia wabunge wakijadili uhaba wa matundu ya vyoo na upungufu wa madawati, badala yake, Bunge lijikite zaidi kujadili mambo mazito kama ya kwenda mwezini na kadhalika.

Profesa Mkumbo aliyasema hayo wiki iliyo-pita wakati akielezea kuhusu kilichomo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa mawaziri na wakuu wa mikoa, ambapo alisema mpango unawataka serikali kuu kuachia udhibiti kwenda chini.

Alisema mpango huo unaeleza wazi kuwa serikali za mitaa ndiyo wasimamizi wakuu wa kila kitu, hivyo walijue hilo.

Alisema ili kupiga hatua haraka za maendeleo, nchi haitaendelea kuwa na Bunge linajadili ujenzi wa matundu ya vyoo pamoja na upungufu wa madawati, kwamba masuala hayo yatajadiliwa ngazi za serikali za mitaa, badala yake bunge linapaswa kujadili mambo makubwa yakiwamo ya kwenda mwezini.

Waziri huyo alisisitiza kuwa mpango huo wa maendeleo wa miaka mitano unaainisha kuwa ni lazima serikali iweke mazingira mazuri ya biashara na kuondoa udhibiti kwenye maisha ya watu.

“Hili inaonekana ni eneo gumu kwa sababu watu tunapenda ku control (kudhibiti), kutoa maelekezo kwa kila mtu, na utasikia wafanya-biashara nao wanasema ‘nimepewa’ maelekezo haya na mkuu wa mkoa.

“Sisi kama viongozi tunatamani kutoa maelekezo kwa kila mtu, hapana, wewe sio

bosi wa kila mtu, na hapa naongea na mawaziri wenzangu, sisi sio bosi wa kila mtu hapa Tanzania.

“Wewe ukiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, wewe ni bosi wa watumishi wa viwanda na biashara, sio bosi wa wenye viwanda, sasa huwa tunajisahau sisi ambao tumepewa madaraka ya kiserikali, tunadhani ni bosi wa kila mtu. Unakuta mtu anafokea na kutoa maelekezo kwa kila mtu, hapana unatoa maelekezo kwa watumishi walioko chini yako tu.

“Kama ni mkuu wa mkoa wa Singida, toa maelekezo ya watumishi wa serikali wa mkoa wa Singida, sasa wewe umekuwa mkuu wa mkoa ni bosi wa kila mtu, mpaka wamiliki wa hoteli, wapi na wapi, hili ndilo tatizo.” alisema Profesa Mkumbo na kuongeza kuwa:

Akitoa mfano, Waziri huyo wa mipango na uwekezaji alisema haitowezekana bwawa la umwagiliaji linajengwa Nkasi, lakini lisimamiwe kutokea Dodoma, hivyo ni lazima zipelekwe fedha sehemu husika.

Alisisitiza kuwa Mpango huo wa maendeleo ya taifa, ni mpango mgumu unahitaji watu wote wawe na uelewa wa pamoja, pamoja na kuondoa vizuizi kila kona, ambapo unatutaka mkulima anapolipia ushuru kwenye eneo moja tayari amelipa nchi nzima.



■ Habari

Samia aipiga jeki Shule ya Polisi K'njaro



Na Mwandsishi WETU, MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 25 kwa ajili ya kuifanyia maboresho Shule ya Polisi Kilimanjaro ambayo inakabiliwa na uchakavu wa majengo

Ikiwa imejengwa tangu 1933, majengo ya mabweni ya wanafunzi, madarasa na nyumba za askari, yameharibika na hayafai kwa matumizi.

Rais Samia ametoa fedha hizo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati wa kikao cha maofisa wakuu waandamizi wa Jeshi la Polisi kilichofanyika mwaka 2024.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi, alieleza kutolewa kwa fedha hizo wakati akizungumza katika ziara ya Kamati ya Kudu-mu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, kutembelea shule hiyo kukagua matumizi ya fedha hizo.

Ni utaratibu wa kawaida kwa kamati za Bunge kufuatilia matumizi ya fedha zinazotole-

wa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

“Rais ameweza kuyafanya haya ambayo wajumbe mmeyashuhudia, ametoa kiasi cha shilingi bilioni 25 ambazo matumizi yake mmeyaona hapa na kwamba fedha zimetumika kwa weledi mkubwa wa Jeshi katika utekelezaji na uwezo wa kusimamia kazi,” alisema Katambi.

Akaongeza; “kukamilika kwa majengo haya, ni sehemu ya miradi mingine ya ujenzi wa nyumba sehemu mbalimbali ambapo mheshimiwa Rais Samia pia anatoa kiasi kikubwa cha fedha na pale Dodoma tayari mradi ushaanza...”

“Miradi yote hii tunatumia wataalamu wetu wa ndani na wanajenga kwa viwango vilevile kama mliyooona Shule ya Polisi. Tunaenda kufanya maboresho ya maslahi kwa askari, mabadiliko ya sera na sheria na teknolojia za kisasa pia zinaendelea kuingizwa jeshini ili vifaa vya kisasa vitumike katika kulinda usalama wetu.”

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Najma Murtaga Giga, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kujenga mradi huo kwa ufanisi na weledi mkubwa huku akikiri kuona thamani ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, ameishukuru Kamati hiyo kwa kutenga muda na kuona umuhimu wa kutembelea Shule ya Polisi Tanzania mkoani Kilimanjaro na kuona thamani ya fedha iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, IGP Wambura, ameambia kamati hiyo kuwa serikali ya awamu ya sita imeendelea kuliwezesha Jeshi la Polisi kwenye miundombinu mbalimbali kote nchini ili kuhakikisha askari wake wanafanya kazi kwenye mazingira mazuri na wezeshi katika kuwahudumia wananchi.

Wambura alisema jeshi lake limekuwa likiendelea na wajibu wake, bila kujali mazingira ambayo yanaweza yasiwe mazuri sana, lakini anatambua juhudi zinazofanywa na serikali kuhakikisha changamoto za askari zinatatuliwa kila inapowezekana kufanya hivyo.

Serikali yafafanua malalamiko ya ‘Dudubaya’

Na Mwandishi WETU

WIKI chache baada ya msanii wa Bongo Fleva, Tumaini Godfrey - almaarufu Dudubaya, kuibua tuhuma dhidi ya Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) kuhusu mashine za MRI, taasisi hiyo imekanusha tuhuma hizo.

Dudubaya katika madai yake alilalamikia ubovu wa vifaa vya hospitali hiyo ya MOI na kutuhumu kwamba vifaa tiba vyake ni vya mtumba.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya amesema tuhuma alizotoa msanii huyo hazina ukweli wowote.

Akitoa ufafanuzi wakati akiwa kwenye ziara ya Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwananyama Machi 13, 2026, Dkt. Ulisubisya amesema mashine za MRI zilizonunuliwa na serikali katika taasisi hiyo ni mpya.

“Mashine zote za MRI zimenuuliwa na serikali zikiwa ni brand new (mpya kabisa), ya kwanza ilinunuliwa mwaka 2014 na iligharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.0, na ya pili imenuuliwa mwaka 2024 ikigharimu shilingi bilioni 2.7 zote ni brand new yaani tulifungua kutoka kwenye karatasi,” amesema.

Dkt. Ulisubisya amesema ni kawaida mashine za aina hizo “kutoa kelele” wakati wa uchunguzi.

Akifafanua zaidi, amesema kelele hizo ni sehemu ya utendaji wa kawaida wa mashine za MRI za aina hiyo

duniani kote.

“Hivyo wagonjwa wanaofanyiwa kipimo hicho hupewa headphones maalumu zinazokuja na mashine hizo ili kupunguza kelele...”

“Vifaa hivyo pia hutumika kama njia ya mawasiliano kati ya mgonjwa na mtaalamu wakati wa uchunguzi,” amesema.

Akifafanua kuhusu muda wa mgonjwa kuka kwenye mashine hiyo, amesema; “Alipokwenda India (Dudubaya) anasema alikaa dakika 15 na huku alikaa dakika 45, lakini mtaalamu anaamua anakupima nini...”

“MRI inaweza kufanya kwa dakika moja... kutokana na utafiti daktari anaohitaji kulingana na ugonjwa alionao mgonjwa, kwa hiyo suala la kusema alikaa muda mrefu hapa MOI ni utafiti ili ugonjwa ujulikane. Lakini tulichokigundua MOI ndio hicho hicho kilichogunduliwa India,” amesema.

Aidha amesema msanii huyo baada ya kupelele majibu ya vipimo vyake, madaktari wakampa sababu ya ugonjwa wake na wakamwambia njia bora ni kufanyiwa upasuaji.

“Lakini kwa hiari yake mwenyewe, akasema hapana angependa kwenda nje ya nchi akapata mfadhili kwa taarifa tulizonazo akaenda India,” amesema.



Mashine ya MRI

■ Makala

Mradi kukomboa wanawake wajasiriamali Zanzibar waja

Katibu Mkuu
Wizara ya
Maendeleo Jamii
Zanzibar, Abeda
Rashid Abdalla



Na Jabir IDRISSA

KATERINA Peter, mjasiriamali mwanamke anayeishi Kianga, Unguja, amezaliwa upya. Taarifa za kuzinduliwa mradi wa kukuza usawa wa kijinsia nchini zimemzidishia ukakamavu, akisema “sasa huenda nitatoboa.”

Amekuwa akijichumia kwa miaka yote 15 ya ujasiriamali akijihusisha na utengenezaji bidhaa mbalimbali za chakula, dawa za kusafisha majumbani na vipodozi.

Tangu alipoanza kwa mtaji wa shilingi 200,000 tu, hadi sasa anapomiliki nyumba ya kuishi na familia, na akisomesha watoto wake, amekuwa kama kuku wa kienyeji – anachakura na kujitafutia chakula na maji kivyake vyake. Hana msaada.

Kwenye mahojiano na Pambazuko hivi karibuni, Katerina anafichua siri asiyowahi kuieleza hadharani. “Unavyoniona amini sijawahi kubahatika mikopo au misaada inayotolewa kupitia mifumo ya serikali.”

Anaeleza hayo akijibu swali kama amewahi kupata mkopo au msaada wowote kutoka serikalini. Katerina anajulikana kijijini kwake, wilaya nzima ya Magharibi A, na miongoni mwa vikundi mbalimbali vya wajasiriamali, hususan vya wana-

wake. Vipo vikundi vinamtambua kwa ukakamavu wake hata kumuita ‘Mama Maarifa.’

Anajulikana anavyojitolea kusaidia wanawake wenziwe kwa lengo la kuhakikisha nao wanapiga hatua ya maendeleo. Mwenyewe haoni kama amefika mbali akiwaangalia wanawake waliofanikiwa katika ujasiriamali na kutamani kuwafikia. Bali si kwa mikopo umiza.

“Nani? Mie kukopa ninaogopa kwa sababu wakopeshaji wengi nje ya serikalini, siku hizi ha-waaminiki,” anasema kwa sauti ya kulalamika.

Ndipo hapa taarifa za tukio la kuzinduliwa mradi wa kitaifa wa kukuza usawa wa kijinsia nchini, zinavyokuja kwa wakati muafaka kwake.

“Hapo patanifaa sana. Ninasubiri hii fur-sa mpya nijaribu bahati. Labda nitatoboa maana nimehangaika kujipa moyo sijafanikiwa. Malengo makubwa na itasaidia jamii ninayoishi nayo wilayani kwetu maana tunaambiwa ukimsaidia mwanamke mmoja umesaidia jamii.”

Mjasiriamali wa mfano huu ndio hasa wali-olengwa na serikali kuwa wanufaika wa mra-di uitwao ‘Pamoja’, uliozinduliwa wiki iliyopita kwenye hafla ya kufana Ukumbi wa Bwalo la Poli-si, Ziwhani, mjini Zanzibar.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Abeda Rashid Abdalla aliyetoa maelezo ya mradi, anasema, “Ni ukombozi kwa wanawake ambao wamekuwa wakikwamishwa na changamoto mbalimbali hasa uwezeshaji. Shughuli zao za kiuchumi zitanufaika.”

Inatarajiwa asilimia 80 ya walengwa zaidi ya 41,000 waliokusudiwa kunufaika na mradi, kuwa wajasiriamali wanawake na tayari wamebainishwa kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi {ZEEA}.

Maeneo ya utekelezaji mradi: Wilaya ya Kaskazini A, B, Kati, Kusini. Kwa Pemba ni Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni. Mradi wa miaka mitano – 2025/2029 unadhaminiwa na Benki ya Dunia iliyotoa zaidi ya shilingi 100 bilioni.

Mradi ulizinduliwa rasmi na Balози Injini Zena Ahmed Said aliyetilia mkazo wanaume kuzinduka na kuacha kuwakwamisha wanawake wanaojitahidi. Waziri Anna Athanas Paul alitoa nasaha mbele ya vikundi vilivyojumuisha wanawake wapatao 500.

Buriani Profesa Costa Ricky Mahalu



Na Aloyce KOMBA

WAKILI msomi mwandamizi, Profesa Costa Ricky Mahalu alikuwa na leseni au usajili wa uwakili namba 477, yaani namba yenye tarakimu tatu.

Huyu ni mmoja wa walimu wakongwe wa sheria nchini Tanzania. Ni rika la Prof. Issa Gulam-hussein Shivji, Prof. Gamaliel Mgongo Fimbo, na Prof Leonard Paul Shaidi.

Prof. Mahalu aliwafundisha pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Kitivo cha Sheria, miaka ya themanini akina Prof. Chris Peter Maina, Prof. Asha Rose Mtengeti-Migiro, Prof. Zebron Gondwe, Prof. Jwani Mwaikusa, Prof. Ibrahim Hamisi Juma (jaji mkuu msataafu), Prof. Luitfried Mbunda, Prof. Palamagamba John Kabudi, Prof. Bonaventure Rutinwa, na Dkt. Sengondo Mvungi.

Wengine ni Dkt. Masumbuko Roman Mahun-

ga Lamwai, Dkt. Ringo Willy Tenga, Dkt. Harrison Mwakyembe na wahadhiri wengine waliotufundisha sisi wa vizazi vya miaka ya tisini na elfu mbili ambao ni majaji, mahakimu na mawakili wa leseni zenye namba za tarakimu nne.

Prof. Mahalu alibobea katika sheria za kimataifa na ndiyo maana alipokuwa balozi katika nchi za Ulaya alikowahi kuishi enzi akisoma na kufundisha, alifanya vizuri katika nyanja ya diplomasia.

Wanafunzi wengine wa Prof. Mahalu ni kaka zangu Prof. Florens Luoga, Dkt. Wilbert Kapinga, Dkt. Mapunda Senior, na Dkt. Mapunda Junior.

Pia kuna yule msomi mwenye akili sana, Robert Makaramba (jaji mstaafu) niliyekuta sifa zake za kitaaluma shule ya Sekondari ya Mzumbe ("O" Level & "A" Level) kwa kufaulu masomo yote ya Sanaa na Sayansi kwa alama za juu mno.

Profesa Mahalu aliiheshimisha na kuipenda sana Tanzania, hasa katika uhusiano na Vatican, pale Makao Makuu ya Kanisa Katoliki Duniani. Vatican ina hadhi ya nchi kamili. Mahalu alikuwa balozi wetu nchini Italia. Ndiyo maana sikushangaa mnamo Machi 9, 2026 kusikia habari za kifo chake zikitangazwa katika vyombo vya habari vya Vatican hususan Vatican News.

Prof. Mahalu amewasaidia vijana wengi wasomi wa sheria kwa kuwafadhili, kuwatia moyo na kuwapa fursa za kazi akiwemo binti yangu, Dkt. Norga Alloyce Komba, aliyesoma shahada ya kwanza na ya pili ya sheria katika chuo kikuu alichokianzisha kikiwa pia na kozi za uongozi cha Bagamoyo ingawa sasa hakipo tena.

Profesa Mahalu alikuwa ni msomi makiini, muungwana, mpole, mwema, mkarimu, mnyenyekevu, muadilifu, mzalendo na mcha Mungu.

Bwana alimtoa Profesa Mahalu, Bwana amemtwa Profesa Mahalu, jina lake lihimidiwe.

■ Makala

Rais Trump aingiwa mchecheto



Na Mwandishi WETU

RAIS wa Marekani, Donald Trump ameanza kupata mshawasha akihofia kuondolewa madarakani kabla hajamaliza muda wake wa miaka minne.

Taarifa iliyochapishwa na Al Jazeera mwishoni mwa wiki inabainisha kuwa rais huyo mbabe ameyonesha wasiwasi wa kuondolewa madarakani iwapo chama chake cha Republican kitashindwa katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika nchini humo mwezi Novemba mwaka huu.

Hata hivyo, rais huyo ametabiri kuwa chama chake kitapata ushindi mkubwa katika uchaguzi huo. Lakini iwapo hilo halitokea, basi anaamini kuwa anaweza kupigiwa kura ya kutokuwa na imani bungeni.

Anaamini kuwa kwa kuwa iwapo Seneti na Baraza la Wawakilishi litakuwa na wajumbe wengi kutokea Democrat, basi safari yake ya urais itaishia hapo.

Ndio maana rais huyo amewaonya wajumbe wa Seneti na Baraza la Wawakilishi wa chama chake kuwa wasipofanya kampeni za nguvu kuna hatari kubwa nao wakaangushwa katika uchaguzi huo na yeye akafuatia.

Akizungumza na watunga sheria hao katika kikao kazi jijini Washington Jumatano iliyopita,

Trump alisisitiza umuhimu wa kupata idadi kubwa ya wajumbe ili kuhakikisha chama hicho kinadhibiti Seneti na Baraza la Wawakilishi.

“Inabidi mfanye kila kitu ili mshinde uchaguzi wa katikati ya msimu kwa sababu msiposhinda watatafuta sababu na watakuwa na nafasi ya kunipigia kura ya kutokuwa na imani na kuniondoa madarakani,” alisema.

Kwa mujibu wa Katiba ya Marekani, Baraza la Wawakilishi lina mamlaka ya kumfungulia mashitaka rais au kiongozi mwingine yeyote mwandamizi kwa matumizi mabaya ya madaraka ikiwemo uhaini, rushwa au makosa mengine makubwa ya kijinai.

Iwapo rais atapatikana na hatia, basi Seneti itamfungulia mashitaka rasmi na kumwondoa madarakani kwa uamuzi ambao unapaswa kuungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe wote.

Katika uchaguzi huo wa Novemba, viti vyote 435 vya Baraza la Wawakilishi vitakuwa wazi kugombea pamoja na viti 33 vya Seneti.

Kwa muda sasa Rais Trump amekuwa akishinikiwa Baraza la Wawakilishi ambalo lina wajumbe wengi kutoka chama chake kupitisha mgawanyo mpya wa majimbo ya wawakilishi ambao utakipendelea chama chake.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya kisiasa nchini humo wanalitaja suala hilo kuwa ni kinyume na misingi ya kidemokrasia.

Majimbo ya Texas, Missouri na North Carolina yameshapitisha sheria ndogo za kuyagawa baadhi ya maeneo ya uchaguzi kama njia ya kukipa chaka cha Republican nafasi ya kupata wawakilishi wengi.

Wakati uchaguzi huo ukikaribia, uungwaji mkono wa Trump umekuwa ukipungua. Kura za maoni za hivi karibuni zinaonesha kuwa uungwaji mkono wa rais huyo mtata ni kati ya asilimia 42 na 45.

Hali inatarajiwa kuwa mbaya zaidi na kuporomoka kwa ushawishi wa Trump hasa kutokana na matukio ya hivi karibuni.

Matukio hayo ni pamoja na kukamatwa kwa nguvu na jeshi la Marekani kwa Rais wa Venezuela, Nicolas Maduro na vita dhidi ya Iran ambayo ime-shaanza kusababisha matatizo makubwa kiuchumi duniani kiasi cha Marekani kuiruhusu Urusi kuuza mafuta yake kwa atakayehitaji.

Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Namna ya kumsaidia mtoto mwenye maumivu

ELIMU ya afya inaweza kupatikana kwa mtu binafsi kutafuta taarifa sahihi za afya, kuzielewa na kutumia taarifa hizo kufanya uamuzi sahihi kuhusu afya yake.

Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza kuwa elimu ya afya ni jambo la kupewa kipaumbele na nchi zote.

Safu hii leo inazungumzia suala la maumivu wanayoweza kupata watoto kwenye miili yao, lengo ikiwa ni kuongeza uelewa kwa wazazi na jamii juu ya mbinu mbalimbali zitakazosaidia kukabiliana na maumivu.

Maumivu siyo dalili nzuri, lakini ina msaada sana kwa binadamu. Tafakari kuhusu mfano huu; Je umewahi kujikwaa, na kidole gumba kikagonga mahali pagumu – ikiwamo jiwe? Hali hii husababisha maumivu, siyo hilo tu, lakini maumivu yalikufanya ujue kuna tatizo na uchukue hatua ikiwemo kutafuta msaada kama maumivu hayaiishi.

Sote tuna wajibu wa kujenga tafsiri sahihi kwa watoto kuhusu maumivu, waelewe ni ishara muhimu mwilini.

Ishara hii inatokana na tafsiri inayofanywa ya ubongo kuhusu hatari mbalimbali zinazotokea kwenye miili yetu.

Ikitokea kama siku chache baada ya kuumia au kupata jeraha, bado unapata maumivu makali, hali hii inatusaidia kujifunza kuwa jambo gani ni sahihi na hili inatuambia mwili unahitaji muda kidogo ili upone.

Kwa watoto, mara nyingine hawana maneno ya kueleza wanavyojisikia “mtu mzima atakuambia mgongo unauma sana,” lakini kwa mtoto utaona ishara, anakuwa kimya, anaacha kucheza kama kawaida, au analialia.

Na nchi yetu kama nchi nyingi za Afrika, mama ndiye mhusika mkuu na anamkemea huyu naye analialia, akimaanisha tujikaze, ni muhimu

kufahamu kutambua changamoto mapema ni hatua ya kwanza na muhimu kwa uponyaji.

Ni muhimu kuzingatia mambo haya pale mtoto anapokuwa kimya na anajitenga kuliko kawaida.

Utamuona anaacha kushiriki michezo anayoipenda na halali kama ilivyozeleka.

Pia, maneno ya kujirudia rudia kama “inauma” ni muhimu kumkagua, uwe mdadisi ni nini hasa kimetokea.

Jamii yetu inaamini dawa za kutuliza maumivu (Mfano. Panadol, Gofen au Diclofenac) ndio mbinu pekee ya kusaidia kukabiliana na maumivu, jambo ambalo si kweli.

Tafti mbalimbali zinaonyesha mbinu mbalimbali tofauti tofauti ambazo hutumika kumsaidia kutuliza maumivu mbali na dawa, lakini pia zinaonyesha athari za matumizi ya dawa kiholela au kwa muda mrefu.

Mpe dawa za kutuliza maumivu inapobidi kwa kufuata mwongozo wa wataalamu wa afya.

Mbali na dawa mbinu zifuatazo zinaweza kumsaidia.

Ni lazima uwe karibu naye kimwili (mkumbatie au mbebe) hii inamfanya atulie, inampa faraja na hunyamza. Hii ni muhimu sana, inatengeneza mazingira salama kiakili na kimwili.

Vyema, ukaacha kumkemea, au maneno kama ajikaze mwache aonyeshe hisia inamsaidia kumfanya ajue namna ya kwanza ya kukabili maumivu si kuyakwepa kwa kujikaza ila kuyakabili kwa namna sahihi.

Tumia vitu vinavyoweza kuondoa akili isiwaze maumivu wakati wote, kama muziki nzuri anazopendelea, mfundishe mazoezi ya kuvuta hewa ndani na kutoa taratibu.

Angalia ni mkao gani ambao haupelekei maumivu zaidi. Mlaze mahali tulivu pasipo na kelele nyingi ili apumzike.

Mbinu hizi na zingine kama kumfanyia massage, au kukanda na barafu mahali palipovimba au maji moto zinaweza kusaidia sana kupunguza maumivu.

Mwandishi ni Ofisa Mfiziotherapia na mwandishi wa Kitabu cha Mbinu za Kutiibu Maumivu Sugu. Anapatikana kwa simu: 0765359305; Instagram: Emmanuel Jacob

■ Kilinge cha Mawasiliano

Na Loth MAKUZA



Vyombo vya habari vihudumie umma, siyo kejeli na mipasho

KATIKA jamii yoyote inayotaka kupiga hatua, wachambuzi wanaotumia redio, televisheni na magazeti wanapaswa kuwa zaidi ya watu wa kujaza muda wa vipindi au kurudia mijadala ya kila siku isiyo na matokeo.

Wanapaswa kuwa daraja kati ya taarifa na uelewa wa wananchi. Hapa ndipo umuhimu wa kuwa na ujuzi wa mawasiliano na umma unapojitokeza.

Mchambuzi mzuri siyo yule anayesema mengi, bali anayeeleza kwa lugha nyepesi, sahihi na yenye kujenga ufahamu juu ya mambo yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja.

Leo hii, sehemu kubwa ya mijadala katika vyombo vya habari imeelemewa na mada za michezo, mitindo ya maisha, ugomvi wa wasanii, maisha yao binafsi na mipasho isiyoisha.

Ni kweli kuwa burudani ina nafasi yake, laki-

ni haiwezi kuchukua nafasi ya mijadala muhimu kuhusu uchumi wa wananchi, ajira, elimu, afya, kilimo, biashara ndogo, bei za bidhaa, uwekezaji, mabadiliko ya tabianchi, usafiri, kodi na huduma za jamii.

Haya ndiyo masuala yanayoamua kama familia itakula, mtoto atasoma, mkulima atauza mazao yake kwa faida au kijana atapata ajira.

Ndiyo maana wachambuzi wanapaswa kujifunza mawasiliano na umma kwa kina. Ujuzi huo unawasaidia kujua namna ya kuzungumza kwa uwazi, kupanga hoja kwa mantiki, kuepuka jaza, na kuwafikia wasikilizaji au watazamaji wa kada tofauti.

Mtu anaweza kuwa na elimu kubwa sana, lakini kama hawezi kuwasilisha mawazo yake kwa lugha inayoeleweka na inayovutia, mchango wake kwa jamii hubaki mdogo.

Vyombo vya habari vinahitaji wachambuzi wanaoweza kufafanua sera za serikali, kueleza bajeti kwa lugha ya mwananchi wa kawaida, kuonyesha fursa za kiuchumi, na kuwasaidia watu kuona namna maamuzi ya kitaifa yanavyoathiri maisha yao ya kila siku.

Tunapopata wachambuzi wenye ujuzi huo, vyombo vya habari hugeuka kuwa chombo cha ukombozi wa kiuchumi.

Mwananchi anapopewa maarifa sahihi juu ya masoko, mikopo, uwekezaji, ufugaji, kilimo bora, teknolojia na ujasiriamali, anawezeshwa kufanya maamuzi bora zaidi. Hapo ndipo redio, gazeti au televisheni inapokuwa shule ya umma, si jukwaa la makelele.

Ni wakati sasa kwa wahariri, watayarishaji na wamiliki wa vyombo vya habari kutafuta na kuendeleza wachambuzi wenye upeo mpana wa masuala ya jamii na uwezo mzuri wa mawasiliano.

Taifa halihitaji sauti nyingi tu; linahitaji sauti zenye maarifa, mwelekeo na dhamira ya kuwainua wananchi.

Vyombo vya habari vikitumika vyema, vinaweza kuwa injini ya maendeleo ya kweli.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz

Barua za Wasomaji ■

**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

**Wenye tabia hizi
wabadilike**

Mhariri,

KUMEKUWA na tabia ya baadhi ya watu kwenye daladala au kwenye msongamano wa watu kukohoa au kupiga chafya bila kufunika mdomo.

Huu siyo ustaarabu kwa sababu wanaofanya hivyo kwa asilimia kubwa wanawaambukiza wengine maradhi yanayoambukiza kwa njia ya hewa bila sababu.

Kwanini mtu asitumie kitambaa au hata viganja vya mikono akitaka kukohoa?

Wenye tabia hizi wabadilike ili kuepuka kuwakera au kuwaambukiza wengine.

Serikali imeshatangaza kuwa kuna maambukizo ya Covid yamerudi, tuwe makini.

**Hassan Hussein,
Kijenge, Arusha.**

**Mtandao wa
kuomba vibali vya
kazi haufunguki**

Mhariri,

NI zaidi ya wiki sasa mtandao wa vibali vya kazi (Work Permit) unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Uhusiano, haufanyi kazi.

Kabla ya kwenda chini kabisa, website ilikuwa taratibu sana, lakini sasa ni zaidi ya wiki haipatikani kabisa na kila tukipiga simu wanasema wanafanya matengenezo.

Hakuna kibali cha kazi kinachoombwa wala kutoka na ukiangalia ni eneo nyeti kwani linahusu wageni na wawekezaji. Hii imekuwa kero kwa watumiaji wengi.

Ni vyema mamlaka zikaeleza iwapo kuna tatizo na tamko rasmi litolewe.

**Ernesto Kapoma,
Wilolesi, Iringa**

Huduma muhimu zisogezwe pembezoni kwa mji

Mhariri,

SABABU kubwa ya foleni katika Jiji la Dar es Salaam ni kwa kuwa huduma zote muhimu kama hospitali, masoko ya jumla, Mahakama, Bandari na ofisi za serikali kukusanyika katikati ya jiji.

Kuwepo kwa huduma hizo muhimu katikati ya jiji, kila asubuhi na jioni, maelfu ya wakazi wa Dar es Salaam ambao huishi nje ya mji husababisha

barabara zote muhimu kufurika magari.

Mfano mzuri ni Jiji la Dodoma ambapo ofisi nyingi za serikali zimejengwa nje ya mji.

Kwa kuwa Dar es Salaam kero hii imekuwa sugu, huduma muhimu zisogezwe pembezoni mwa mji.

**Ally Hhayuma
Tegeta, Dar es Salaam**

Na Rashid MTAGALUKA



Hoja Yangu ■

Kupanda kwa dola, nani anaumia Tanzania?



ASUBUHI moja mfanyabiashara wa vifaa vya umeme eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, anatazama bei mpya za bidhaa kutoka nje.

Wiki iliyopita aliagiza bidhaa kwa dola za Marekani 1,000. Leo anapopiga hesabu, anaona gharama imeongezeka kwa sababu thamani ya shilingi imepungua kidogo dhidi ya dola.

Anatikisa kichwa na kusema; “hii dola ikipanda kidogo tu, sisi wafanyabiashara tunahisi mara moja.”

Kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania, Shilingi ya Tanzania imekuwa ikibadilika thamani katika miezi ya karibuni kutokana na mahitaji makubwa ya dola katika soko.

Mwanzoni mwa mwaka huu 2026, thamani ya shilingi ilishuka kutoka takribani shilingi 2,450 kwa dola hadi zaidi ya shilingi 2,534 kwa dola katika kipindi cha wiki chache tu.

Kwa maoni yangu, wafanyabiashara wanaotegemea bidhaa kutoka nje ndio kwa kiasi kikubwa waathirika namba moja katika hili.

Hii ni kwa sababu Tanzania inaagiza bidhaa nyingi muhimu kama mafuta, mashine za viwandani, vipuri vya magari na hata baadhi ya vyakula. Wakati dola inapopanda, gharama za kuagiza bidhaa hizi huongezeka mara moja.

Mfano mzuri ni mafuta. Mafuta hununuli-

wa kwa dola katika soko la dunia. Ikiwa dola inapanda, gharama ya kuagiza mafuta pia inapanda, na hatimaye gharama hiyo huonekana kwenye bei ya usafiri na bidhaa sokoni.

Athari ya pili inawagusa wananchi wa kawaida. Wakati wafanyabiashara wanapounua bidhaa kwa gharama kubwa, hulazimika kuongeza bei. Hivyo hata mama anayenunua sukari au unga sokoni anaweza kulipa zaidi bila kujua sababu ya msingi ni kupanda kwa dola.

Hata hivyo, kuna upande mwingine wa sarafu. Wataalamu wa uchumi wanaeleza kuwa hali hii mara nyingi ni ya msimu.

Mapato ya dola nchini hupungua kati ya Januari na Mei kwa sababu sekta kama kilimo, utalii na madini huwa katika kipindi cha mapato madogo.

Wakati huo huo mahitaji ya dola yanaongezeka kutokana na wafanyabiashara kuagiza bidhaa kutoka nje.

Ili kupunguza presha hiyo, Benki Kuu ya Tanzania mara kadhaa imeingiza dola katika soko la fedha za kigeni. Mapema Machi 2026 benki hiyo iliingiza dola milioni 20 ili kuongeza upatikanaji wa fedha hizo na kusaidia utulivu wa soko.

Hoja Yangu hapa ni juu ya mafunzo makubwa kwa uchumi wa Tanzania yanaonekana wazi, kwamba kadiri nchi inavyotegemea bidhaa kutoka nje, ndivyo dola inavyokuwa na nguvu kubwa katika maisha ya kila siku ya wananchi.

Suluhisho la muda mrefu linaweza kuwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa ndani, kukuza viwanda na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi.


Kwa sababu tuendako, nguvu ya shilingi haitategemea maamuzi ya benki kuu pekee, bali pia uwezo wa uchumi wa Tanzania katika kuzalisha na kuuza zaidi duniani.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Jinsi ya kusoma Pambazuko ■



Soma Gazeti la Pambazuko Popote Ulipo!



Scan QR Code
Kusoma


Jinsi ya Kusoma Pambazuko Ndani ya Rifaly

- **Scan QR Code** – Itakupeleka moja kwa moja kwenye channel ya Pambazuko ndani ya Rifaly.
- **Jisajili au Ingia (Log In)** – Tumia namba ya simu, barua pepe, au akaunti ya Google.

Furahia Kusoma Pambazuko muda wowote na mahali popote ulipo.



Pakua Rifaly Sasa
na Anza Kusoma



Fanya haya kuponya ndoa yako

HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Karibu uweze kujipatia maarifa mbalimbali.

Wiki hii nitazungumza namna ya kuyafanya maisha ya ndoa kuwa na furaha.

Furaha ndani ya ndoa ni matokeo ya juhudi na kujitolea kati ya mume na mke kwa kudumisha njia zifuatazo;

Mawasiliano - mawasiliano ya wazi na ya uaminifu ni muhimu hivyo wanandoa mnapaswa kuzungumza kuhusu hisia zenu, mahitaji, na matarajio.

Maelewano - hapa mnapaswa kuelewana na kuthamini tofauti zenu na kuzirekebisha ili kusonga mbele.

Kushirikiana - hapa mnatakiwa kufanya uamuzi na kutatua matatizo yenu kwa pamoja.

Nyingine ni kila mmoja wenu kujali hisia na

mahitaji ya mwenzake, kusameheana na kusahau yaliyotokea na kubwa katika yote ni kuzidisha upendo kati yenu siku hadi siku.

Wanandoa au wapenzi wanatakiwa kutenga muda wa pamoja kufanya mambo mnayoyapenda (hapa mnaweza kwenda sehemu za starehe na kubadilishana mawazo).

Jambo jingine ni kushughulikia migongano kati yenu kwa amani na heshima bila kuathiri uhusiano wenu au familia lakini pia mkosaji kukubali kubadilika na kuwa tayari kubadilika kwa ajili faida ya ndoa yenu.

Maisha ya ndoa hivi sasa yamekuwa na changamoto kiasi cha kusababisha ndoa nyingi kusambaratika na hadi kufikia hatua ya kuvunjika. Ili kurekebisha hali hiyo wanandoa wapaswa kushughulikia matatizo yao kwa njia ya staha kuliko vinginevyo.

Wanandoa kumbukeni kuwa muungano wenu ni safari ya pamoja, hivyo ni muhimu kufanya kazi pamoja ili kuifanya ndoa yenu iwe ya furaha.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■

Mambo matano ya kuzingatia unapovaa hijab

KULINGANA na utamaduni wa dini ya Kiislamu, wanawake wanapaswa kufunika kichwa kwa kuvaa hijab au kwa kufunga kilemba.

Katika kipindi cha mfungo wa Ramadhani, wanawake wa dini hiyo hata wale ambao walikuwa hawajazoea kufunika vichwa, huwa wanafunika.

Mambo ya kuzingatia unapofunga hijab;

* Chagua kitambaa kinachofaa au kinachoweza kupumua kama vile pamba.

* Chagua mtindo unaokufaa: Jaribu kufunga hijab yako kwa mitindo tofauti kama vile muonekano wa kawaida wa kukunja, kilemba au kubana na pini ya hijabu na kuzungusha au kuachia. Kisha pata kile kinachofaa zaidi kwa sura ya uso wako na mtindo utakaokupendeza.

* Tumia pini za hijab zinazolingana na rangi yako ya hijab ili kuepuka pini zinazoonekana. Unaweza pia kutumia pini za sumaku kufungia hijabu au mitandio kwa usalama zaidi.

* Cheza na rangi na nguo: Ongeza uhusika kwenye vazi lako ukitumia rangi ya nguo na kulinganisha hijab na mapambo yako mengine.

* Mazoezi huleta ukamilifu: Usivunjike moyo ikiwa inachukua muda kufahamu namna ya kufunga hijabu.

Tazama mafunzo ya video, fanya mazoezi mara kwa mara na utayafahamu baada ya hapo hutasumbuka tena.

Zingatia haya kutoa weusi vidoleni

WATU wengi wanaotumia cream kali wamekuwa na changamoto ya kuwa na mabaka meusi kwenye vidole vya mikono na miguu.

Kama una changamoto hiyo na unataka uonekane kuwa na rangi moja mwili mzima zingatia yafuatayo;

Kwanza uwe na kahawa, ndimu na baking powder.


Jinsi ya kufanya;

Chemsha maji kisha yaweke kwenye beseni halafu weka kahawa kijiko kimoja, baking powder kijiko kimoja na ukamulie ndimu.

Baada ya kuloweka mchanganyiko huo kwa dakika moja, hatua inayofuata anza kujisugua vidole vyako kwa muda wa dakika 5, baada ya hapo nawa mikono yako kwa maji ya uvuguvugu.

Ukimaliza zoezi hilo kausha mikono yako vizuri kisha upake mafuta ya maji yawe ya nazi au mzaituni.

Fanya zoezi hilo usiku muda unaokwenda kulala. Kwa matokeo zaidi ufanye kwa wiki mbili mfululizo.



■ Burudani



Frida Amani ahamasisha utunzaji mazingira

Na Mwandishi WETU

BALOZI wa Mazingira ambaye pia ni msanii na mtangazaji, Frida Amani ametembelea Shule ya Sekondari Abbas Tarimba kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa utunzaji mazingira.

Frida ambaye pia ni Mkurugenzi wa The Amani Foundation, amesema vijana wa leo ndio mabalozi wa kesho katika uhi-fadhi wa mazingira.

Kutokana na hilo, amesema ni muhimu kuwajengea uelewa mapema ili wawe sehemu ya suluhisho katika kulinda mazingira yanayowazunguka.


Kupitia taasisi yake hiyo ya Amani Foundation, ameeleza kuwa ziara hiyo ni mwanzo wa kuwafikia wanafunzi katika shule mbalimbali nchini. "Ziara hii ni mwanzo wa kuhamasisha wanafunzi wengi zaidi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na namna wanavyoweza kushiriki kikamilifu katika juhudi za kuyahifadhi mazingira," amesema Frida

Rihanna akimbia nyumba yake


Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI wa Pop na RnB kutoka Marekani, Robyn Rihanna Fenty - almaarufu Rihanna, amechukua uamuzi wa haraka kwa kuhama baada ya nyumba yake iliyopo Los Angeles, kupigwa risasi Jumapili iliyopita.

Mizigo ya Rihanna ilionekana ikipakiwa kwenye magari na kuendeshwa hadi Uwanja wa Ndege wa Van Nuys. "Kama unavyojua, mamlaka inaendelea kuchunguza kisa cha ufyatujaji wa risasi kilichotokea nyumbani kwa Rihanna Jumapili akiwa ndani na watoto wake..." "Kupitia hili Rihanna ameamua kukaa mbali na eneo la tukio kwa usalama wake," ripoti zinasema.



VITABU... VITABU... VITABU



Je, wewe unapenda kujifunza na kupata uelewa wa mambo anuani?

Kama jibu ni ndiyo, basi kuwa tayari kupata nakala yako ya vitabu vifuatavyo kutoka kwa mwandishi **Simon Martha Mkina;**

1. **Mwalimu Nyerere Hazina Tanzania**
 - Kitabu hiki kilichapishwa mara ya kwanza 1999 mara baada ya kufariki kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sasa kinachapishwa kwa kurejerewa na kuwemo kwa mambo kadhaa ambayo hayakuwahi kuwemo kwenye kitabu cha awali.
2. **Ink meets Mic meets Camera: A Journalism Primer**
 - Kitabu hiki kinachapishwa kwa mara ya kwanza ikiwa ni mwongozo wa mafunzo kwa waandishi wa habari wapya na hata wale wanaotaka kujifunza zaidi kuhusu umahiri katika uandishi wa habari wa magazeti, redio, blog, televisheni (ikiwamo zile zinazotangaza mitandaoni).

Nini kifanyike: Ikiwa utapenda kupata nakala ya vitabu hivi - au kimoja wapo, unatakiwa kuandika ujumbe mfupi kwenye simu yako na kutuma kwa namba hii:

0754 020880. Taja kitabu unachopenda kukipata mara baada ya kuanza kuuzwa.

Vitabu hivi vitauzwa kwa njia ya upekee kwa wale wanaoandika ujumbe kwanza kabla ya kuanza kuuzwa kwenye maduka ya vitabu Tanzania nzima. Bei ya kitabu kuhusu Mwalimu Nyerere ni


Shilingi 20,000 na kile cha mafunzo ya uandishi wa habari ni **Shilingi 30, 000.**

Karibuni sana tuendelee kujifunza.

Elimu ni bahari!



Arsenal waona mwanga wa ubingwa



Na Mwandishi WETU

SASA inawezekana kabisa kwamba 'Washika Mitutu' wa London, ndiyo mabingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2025/26.

Hii inatokana na rekodi na hesabu za mpira zinazopigwa na Klabu ya Arsenal, ambayo msimu huu inaendelea kuonyesha kiwango kikubwa cha soka.

Baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Everton juzi katika Uwanja wa Emirates, Arsenal wamefikisha pointi 70 baada ya mechi 31, huku wakisalia na michezo saba ya kumaliza msimu.

Manchester City, wapinzani wao wakuu, wana pointi 61 baada ya mechi 30 kufuatia sare ya 1-1 dhidi ya West Ham, maana yake Arsenal wako mbele kwa pointi tisa, ingawa City wana mchezo mmoja mkononi.

Hiyo ndiyo sababu kubwa inayofanya mashabiki wa 'Washika Mitutu' hao waanze kuona harufu ya kombe.

Tofauti na misimu iliyopita ambako Arsenal walionekana kuanza kwa kasi kisha kuporomoka mwishoni, safari hii wameonyesha tabia ya timu yenye ukomavu wa ubingwa.

Huenda hawajawa timu ya kuvutia kila dakika machoni mwa wachambuzi, lakini wamekuwa timu inayojua namna ya kushinda, hata pale mambo yanapokuwa magumu. Huo ndio utofauti wa mabingwa na washindani wa kawaida.

Dhidi ya Everton, Arsenal hawakupata ushindi wa kishindo cha mapema, lakini walionyesha subira, nidhamu na imani hadi dakika za mwisho.

Viktor Gyokeres alifunga bao la kwanza dakika ya 89 kabla ya kijana Max Dowman kufunga la pili muda wa nyongeza na kuwa mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Ligi Kuu England.

Ushindi huo haukuongeza tu pointi tatu muhimu; uliimarisha pia hisia kwamba kikosi cha Mikel Arteta sasa kina nguvu ya kisaikolojia ya kubeba presha ya hatua za mwisho za mbio za ubingwa.

Kilichobaki kwa Arsenal ni kutokulewa sifa na kuendelea kucheza kwa nidhamu ileile iliyowafikisha hapa.

Ni kweli wana mechi saba tu, na ni kweli wakishinda mfululizo watajiweka kwenye nafasi kubwa mno ya kutwaa taji.

Hata hivyo, kwa kuwa City bado wana mchezo mmoja zaidi, hesabu hazijafungwa rasmi, lakini ukweli mmoja unabaki; njia ya Arsenal imefunguka, mlango wa ubingwa umeachwa wazi, na sasa ni juu yao kutembea kwa uthabiti hadi mwisho na kuondoa kabisa simulizi ya kwamba wao huanguka kila msimu unapokaribia kufungwa.